




Nefi Anasali kwa ajili ya Watu

Unaweza kusoma hadithi hii katika
Helamani 7:10-17 na 8:7-10.



Nefi alikuwa nabii. Alipewa jina kama jina la Nefi aliyepata mabamba ya shaba. Alikuwa na wasiwasi kuhusu watu. Walikuwa wameacha kumfuata Mungu.



Nefi alikwenda kwenye bustani yake. Alipanda juu ya mnara katika bustani yake na alisali kwa Mungu. Alisali kwa ajili ya watu.



Baadhi ya watu walimwona Nefi juu ya mnara. Walisimama kusikiliza na waliwakusanya wengine kusikiliza. Nefi alipomaliza kusali, aliwaona walikuwa wanaangalia na alianza kuwafundisha.



Nefi aliwaomba watu kutubu. Baadhi yao hawakupenda kile Nefi alichofundisha. Lakini wengine wengi walisikiliza! Walichagua kutubu na walibadilisha njia zao. ●

VIELELEZO NA ANDREW BOSLEY